HIDAYA YA ZANZIBAR

NGANO ZETU ASILIA

BURUDIKA NA KISWAHILI

Yussuf S Hamad

MEI, 2008

STANFORD UNIVERSITY, 2007/08

AJIZI AJIZI

Hapo zamani za kale aliondokea nyuki na familia yake. Baba nyuki na mama nyuki walikuwa na watoto watatu; nyuki, uvi, na duduvule ambae kwa jina maarufu alijulikana kama zenengo. Baba nyuki alikuwa mwalimu mkuu wa chuo kikuu cha kutengeneza asali. Yeye alikuwa fundi na mwanataaluma aliebobea katika taaluma ya utengezaji asali. Alikuwa mtu mzuri; mchapakazi, mchangamfu, mwamiminifu, mcheshi, na mwenye hekima na busara ya hali ya juu. Wakati anakaribia kuwa mzee sana aliwaita watoto wake nakuwaasa. Aliwaambia; ``Enyi wanangu! Mimi baba yenu. Sina nguvu tena kwa sababu nimenza kuwa mzee. Kwa hivyo nakuombeni sana mujitahidi kusoma.elimu ni dira ya mwelekeo wenu na mafanikio yenu kimaisha. Kwa hivyo kuanzia sasa nawataka mujiunge na darasa langu la utengenezaji wa asali. Baba nyuki alimaliza na watoto wote waliitikia.

Siku ilyofuata nyuki mdogo alikuwa wa mwanzo kumka kwenda darasani. Uvi alikuwa hataki kwenda darsani kwa sababu alipenda kukaa na mama yake jikoni muda wote.Uvi alikuwa napendwa sana na mama yake kwa hivyo alidhani mama yake atamsaidia siku zote maishani. Kwa upande wapili zenengo alikuwa kijana wa makamo aliependa starehe na anasa. Yeye aliamka asubuhi na kubadilisha nguo kila mara; asubuhi, mchana, na jioni. Alipenda kuvaa ngu za rangi nyingi nyingi kwa wakati mmoja. Mara nyingi alipenda kuvaa nguo za rangi ya buluu kwa weusi, njano, na samawati baadhi ya wakati. Baada ya kuvaa nguo zake na kujiona amependeza hutoka nyumbani na kwenda kuranda huku na huko kwenye starehe.

Nyuki mdogo aliendelea kusoma kwa baba yake kwa juhudi sana. Kila siku alikwenda darasani na kusoma. Huko shuleni alisomeshwa na baba yake jinsi ya kutengeneza asali. Alisoma kwa bidii na alikuwa mawanfunzi hodari sana. Uvi alikaa na mama yake na baadhi ya siku alikwenda darasani kusoma ijapo kuwa alikuwa haandiki wala kufanya kazi.Zenengo alikuwa haendi kabisa shule.alipoulizwa na marafiki zake kwanini hataki kujifunza ujuzi aliokuwa nao baba yake alijibu; ``ujuzi uko nyumbani siku nikuihitaji basi nitaupata.Ninajuwa baba yangu atanifundisha siku nikiwa tayari.''

Siku moja wakati zenengo ametoka baba nyuki alifariki dunia hafla. Zenengo aliporudi aliona watu wengi wakisubiri kumzika baba yake. Zenengo alisikitika sana. Baada ya mazishi ya baba yake zenengo hakuambulia kitu.yeye alibaki kuhangaika huku na huko kwenye maua akitafuta ua ambalo angeweza kutengeneza asali. Hivyo alikuwa anaruka kutoka ua moja kwenda jengine akisema; `` labda ni hili, labda ni lile, labda ni yale!''. Kisha jioni narudi nyumbani anakutia hana kpa kulala kwani hakuweza kujitengenezea sega. Hivyo akaishia kulala kwenye gogo. Uvi aliechelewa kusoma aliishia kutengeneza sega tu bila kujua kutia asali. Lakini nyuki aliweza kutengeneza asali na alikuwa na nyumba nzuri kwa sababu alisikiliza ushauri wa baba yake. Kuna msemo wa Kiswahili usemao;``Ajizi ajizi utalala mlango wazi``

ARUBAINI YA SUNGURA

Hapo zamani za kale walikuwepo wanyama mbalimbali ambao waliishi kwa pamoja na kushirikiana kwa kila kitu. Siku mmoja Simba; mkuu wa wanyama aliitisha mkutano wa wanyama wote. Wanyama wote wailitikia wito.Siku ya kikao ilipofika wanyama wote walihudhuria katika mkutano huo muhimu wa wanyama. Simba alihutubia wanyama wote na kuwataka wachimbe kisima kwa sababu kulikuwa hakuna maji katika mito na maziwa. Wanyama wote walikubali rai hiyo ya mfalme Simba. Siku ilipofika wanyama wote walikutana na kuanza kuchimba kisima isipokuwa sungura tu. Sungura hakutaka kushirikiana na wanyama kuchimba kisima.Fisi alitumwa na mfalme simba akamuulize sungura kwanini hakuja kushiriki katika kuchimba kisima.

Fisi alikwenda hadi nyumbani kwa sungura. Huko alimkuta sungura akiwa barazani akichambuwa karanga kwa ajili ya chakula chake cha mchana. Fisi alimsalimia sungura; ``Hujambo sungura?'' Sungura alinyanyua uso wake na kumtazama fisi kisha akaitikia ``Sijambo fisi. Habari za siku nyingi?'' Fisi nae aliitikia kwa kusema; ``Mimi sijambo pia! Ila tu nimetumwa nije kukuuliza kwa nini hujashiriki katika ujenzi wa kisima?'' Fisi alimuuliza sungura.Sungura nae alicheka kidogo kisha akamwambia fisi; ``Mimi sina haja ya maji kwani nina maji yangu matamu sana. Maji mnayochimba yana matope na ni machafu. Mimi sipendi maji yenye matope. Nyinyi chimbeni kisima na mimi sitokunywa kamwe maji yenu hayo machafu!''

Fisi aliondoka nyumbani kwa sungura na kuelekea kwa mfalme Simba. Alipofika alimweleza yote aliyoelezwa na sungura. Simba alisikitika sana aliposikia majibu ya sungura ambayo yalijaa kebehi na dharau kwa wanyama wengine. Lakini simba hakumchukulia sungura hatua yoyote. Baada ya siku kupita kisima kilimalizika na wanyama walianza kutumia maji. Kisima kilitoa maji mengi sana na wanyama wote walifurahi. Baada ya siku tatu tu tangu kisima kimalizike na watu waanze kuchota maji wanyama waligunduwa kitu amabacho si cha kawaida pale kisimani. Kila wakifika kisimani asubuhi waliona maji yamechafuliwa sana na kuingizwa takataka nyingi. Hivyo wanyama walimwambia Simba kuhusu uharibifu huu.

Simba alifika kisimani siku iliyofuata na kuona maji yamechafualiwa sana. Simba aliamuwa kuweka ulinzi pale kisimani ili kumkamata anaeharibu maji. Hivyo zamu ya kulinda kisima ikapangwa. Mnyama wakwanza kuanza kulinda kisima alikuwa tembo. Tembo alilinda kisima usiku na alikuwa amejificha kichakani kumdoea mchafuzi wa maji kisimani. Ilipofika usiku wa manane, Tembo alisikia kiumbe fulani kinakuja. Tembo alikaa tayari kumkamata mchafuzi wa maji.Mnyama huyo alikuja hadi kisimani na alikuwa Sungura. Sungura alichota maji, kisha akakoga na baadae akaanza kuyachafua. Tembo alitoka kichakani na kumshika Sungura. Tembo alimwambia Sungura;``Leo nimekushika mchafuzi wa maji. Sikuachi hapa mpaka asubuhi nikupeleke kwa mfalme Simba ili ukapate adabu.'' Sungura alicheka sana na kumwambia Tembo; ``Mimi sio muharibifu wa maji.Kwanza mimi sinywi maji haya. Maji haya si safi na wala si matamu. Mimi nina maji yangu matamu sana.'' Sungura alitoa kichupa kidogo cha asali. Kisha akamwambia Tembo;`` Unaona haya ndio maji

ninayokunywa mimi. Haya ni matamu sana.'' Tembo alishangaa sana na alimwambia Sungura tafadhali nionjeshe kidogo maji yako.'' Sungura alimuonjesha Tembo ile asali ambayo alidai ni maji. Tembo alionja kidogo na kwa vile ilikuwa tamu alimwambia Sungura;'' Tafadhali niongeze tena''. Sungura alimwambia Tembo; ``Hapana! Siwezi kukuonjesha mpaka nikufunge katika mti kwani utanizidi nguvu na kuninyang'anya maji yangu matamu''. Tembo alikubali na Sungura alimfunga Tembo katika mti mkubwa halafu akamcharaza viboko mpaka Tembo alikaribia kufa. Hapo sungura alimwambia Tembo nitakuachia lakini usimwambie mtu kuhusu mimi. Tembo alikubali na Sungura aliondoka na kumwacha Tembo akiwa amefungwa pale mtini. Asubuhi wanyama walipokuja walimkuta Tembo amefungwa amelala akiwa taabani. Walimuuliza kulikoni lakini tembo hakusema kitu.

Siku iliofuata ilikuwa zamu ya Fisi. Nae alipata kipigo kama Tembo, kisha akaja punda ambae pia aliambulia kipigo. Wanyama wote waliopangwa walipigwa sana na Sungura.Akawa amebaki kobe. Kobe alimwambia Simba mimi nitaweza kumkamata mchafuzi wa maji. Wanyama wote walishangaa na kumwambia kuwa hataweza kwani wameshindwa wanyama wakubwa hivyo yeye hatoweza. Kobe alisema nitaweza na alikwenda kisimani. Alipofika alijipaka ulimbo mgongoni kwake. Sungura alipofika hakujua kuwa alikuwepo kobe hivyo aliona kuna jiwe tu pale kisimani. Sungura alipanda juu ya mgongo wa kobe. Mara miguu yake iliganda.Sungura akasema; ``Umeikamata miguu yangu sio? Nina mikono pia''. Sungura alipeleka mikono yake. Mikono ikanasa katika ulimbo na sungura akawa hawezi kutoka.asubuhi wanyama walipokuja walimkuta kobe akiwa ameganda mgongoni kwa kobe hana la kufanya. Kobe alimkabidhi sungura

kwa samba kwa ajili ya kuhukumiwa. Wanyama wote walimpongeza Kobe kwa kazi yake nzuri.

KARAMU YA BUNUWASI

Hapo zamani za kale aliondokea Abunuwasi. Abunuwasi huyo aliishi katika mji mmoja wenye watu kidogo. Katika mji huo Abunuwasi alikuwa mtu maarufu sana kwa sababu alikuwa mcheshi, mchangamfu, na mtu wa masihara sana. Alipenda kucheza na kufurahisha watu. Abunuwasi alijulikana na kila mtu.

Siku moja Abunuwasi aliota ndoto. Katika ndoto hiyo aliota kuwa babu yake aliefariki miaka mingi amekuja kumpa ujumbe. Ujumbe huo ulikuwa anamtaka Abunuwasi afanye karamu kubwa. Katika karamu hiyo Abunuwasi alitakiwa achinje ng`ombe mkubwa na kupika wali mwingi. Kisha alitakiwa awatafute vipofu arubaini katika mji ule waje kula chakula hicho. Bahati mbaya yule babu yake hakumwambia Abunuwasi wapi atawapata vipofu hao arubaini.

Asubuhi Abunuwasi aliamka na kujiuma kichwa. Alijiuliza maswali mengi kisha akasema;`` Ndoto hii lazima iatakuwa ya kweli. Babu yangu hawezi kuja usingizini akaniambia uongo. Huu ni ukweli. Lazima niifanyie kazi haraka. Sasa nitatafuta mchele na yule ng`ombe wangu mkubwa nitamchinja kwa ajili ya karamu. Sawa!``.Baada ya

hapo Abunuwasi alimaliza. Siku ile Abunuwasi alikwenda madukani kutafuta mchele. Kisha alimchukuwa ng`ombe wake mkubwa na kumuweka tayari kwa ajili ya shughuli. Lakini Abunuwasi alikuwa hajuwi wapi atawapata vipofu arubaini kwa sababu katika mji ule kulikuwa na vipofu wasiozidi watano. Abunuwasi hakukujuwa la kufanya.aliendelea tu na matayarisho ya karamu mpaka alipokamilisha kila kitu.

Siku ya karamu ilipofika Abunuwasi alipita mji mzima na kunadi karamu yake. Alikuwa akisema;``Hee! WANANCHI! leo ni leo asie mwana aeleke jiwe. Kutakuwa na karamu ya kukata na mundu nyumbani kwangu leo. Karamu hii ni maalumu kwa watu maalumu. Wahusika wote watapewa kadi za mwaliko. Kila atakaepata kadii ya mwaliko anaombwa kufika mapema bila kuchelewa.`` Abunuwasi alimaliza. Baada ya kutoa tangazo Abunuwasi alikata vipande vidogo vidogo vya karatasi. Vipande hivyo vilikuwa ni kwa ajili ya mualiko. Kisha alichukuwa ngozi ya ng`ombe na kuanza kuiburura mitaani. Kila alipopita watu walimshangaa. Wengine walimuuliza `` Abunuwasi unaburura nini?``. Abunuwasi hakujibu kitu ila alikuwa akimpa kadi ya mwaliko kila alieuliza suali hilo. Baada ya muda kupita karamu ilikuwa tayari kuliwa. Abunuwasi nae alimaliza kutowa kadi zake zote.

Wakati wa kula ulipofika,kila aliepewa kadi ya mwaliko alikuwa amehudhuria. Hapo Abunuwasi aliwakaribisha chakula. Watu walianza kula mpaka wakashiba.Walipomaliza kula Abunuwasi aliwashukuru sana na aliwambia;``Nawashukuru sana nyote mliohudhuria katika karamu hii. Kwani kabla a hapo nilikuwa sijui la kufanya. Nilitakiwa nifanye karamu hii na kuwaalika vipofu wa mji huu waje kula.Kama mnavyojuwa ndugu

zangu mji huu hauna vipofu wengi au pengine wapo lakini hatuwajui.Sasa mimi niliposhindwa nilipita na hii ngozi.Sasa ninafahamu kuwa kila mtu anajuwa kuwa hii ni ngozi au sio?``.Watu waliitikia kwa pamoja ``Hiyo ni ngozi``.Abunuwasi aliendelea;``Sasa nilipoanza kuburura ngozi hii kuna watu waluniuliza; ``Hiyo nini Abunuwasi?``.Mimi sikuwajibu sababu nilijuwa hao walikuwa hawaoni hivyo niliamuwa kuwaalika kama nilivyoelekezwa na babu yangu. Watu wote walishangaa!

KITATANGE

Huko baharini kuna samaki mdogo, mlaghai, mjanja, na mwenye kila aina ya visa na mikasa.Samaki huyo au kisamaki; kutokana na udogo wake, anajulikana kama Kitatange. Kitatange ana tabia ya kuishi huku na huko baharini. Huweza kuonekana maji ya kina kifupi na wakati mwengine maji ya kina kirefu. Kitatange mara nyingi hapendi kutembea na wenzake. Ikitokea akitembea na samaki wengine basi ujue kuna jambo.

Kitatange hupenda sana kuwalaghai samaki wenziwe baharini. Siku moja kitatange alitembelea kundi kubwa la samaki wa kimo cha kati na kati ambao mara nyingi wavuvi hupenda kuwavuwa. Kitatange aliwambia wenzake samaki hao: ``Mnajuwa rafiki zangu? `` . Wale samaki walisimama na kumsikiliza. Mmoja wa wale samaki alimwambia kitatange ``Kuna habari gani njema ewe Bwamdogo! Hebu tueleze``. Kitatange aliwaambia wale samaki; ``Mimi ni mtumishi wa mungu. Kazi yangu nikuhakikisha kuwa viumbe wote wanaishi maisha bora bila upendeleo, ubaguzi, na

wala uonevu wa aina yoyote. Sasa mimi ninawaambia kuwa nimeona chakula kingi katika magari yaliyoshushwa na mungu huku baharini kwa ajili yetu. Mnaonaje tukienda kula chakula hicho pamoja?.Kitatange aliwauliza.Wale samaki walikubali na kumfata kitatange.

Kitatange aliwachukuwa samaki wale kundi zima hadi kwenye mitego ya kutegea samaki.Mitego hii inaitwa dema.Hapo waliona chakula kingi kwenye hayo madema.Samaki wengi katika kundi lile waliogopa kuingia kwani waliogopa.Kitatange aliwambia rafiki zangu msiogope kabisa.Mimi nitakuwa wa mwanzo kuingia humu katika dema.Kitatange aliingia na kuanza kula.Samaki wengine walifatia.Mara waliingia katika dema wote na kunza kula chakula

humo.Baada ya kushiba vizuri samaki walitaka kutoka.Walimtafuta kitatange humo demani.Kitatange alikuwa ameshapenya na kutoweka.Dema lile lilikuwa na tundu ambazo samaki wadogo wanaweza kutoka lakini samaki wakubwa hawataweza kutoka kamwe.Kitatange alikimbia na kuwaacha samaki wengine humo demani. Mvuvi alipokuja siku ya pili alikutia samaki wengi wakiwa ndani ya dema. Alifurahi sana.Aliwavuwa na kuondoka nao wote.

KOROSHENI

Hapo zamani za kale alikuwepo kijana mmoja aliyeitwa Korosheni. Korosheni alikuwa kijana mrefu na mwembamba. Alikuwa mvivu na mjanja sana kwa sababu alikuwa mvivu hakuweza kufanya kazi. Korosheni alikuwa hapendi kufanya kazi yeyote. Yeye aliishi kwa mbinu za ujanja, ulaghai, na hila maisha yake yote.

Siku moja jioni Korosheni alitembea kwa mguu masafa marefu kutoka mjini kwenda kijijini. .Huko kijijini hakuwa na rafiki wala jamaa yeyote. Kutokana na uchofu wa kutembea kwa mguu Korosheni alihisi njaa kali na kiu. Pia alikuwa hawezi kuendelea na safari yake zaidi kwa sababu alikuwa amechoka sana na alihitaji kupumzika.hivyo alisimama katika nyumba moja huko kijijini. Alibisha hodi mara tatu na mara mlango ulifunguliwa. Katika nyumba ile kulikuwa na mwanamke mmoja na mume wake ambao walikuwa ni wakulima na wafugaji. Wao walikuwa na mashamba mengi na mifugo ya kutosha. Kwa sababu walikuwa na wanyama wengi na mashamba walikuwa na chakula cha kutosha pia. Watu hawa walikuwa wakarimu sana. Walimkaribisha Korosheni. Walimpa chakula na sehemu ya kulala pia.

Baada ya kumaliza kula na kupumzika, Korosheni alitoka nje ya nyumba kujipumzisha. Mara alipita bata. Korosheni alipiga kelele sana.Nakufaa! Nakufaa! na mara yule mkulima na mke wake walikuja kumuuliza Korosheni kulikoni. Korosheni alisema;``Mimi ninaogopa sana hawa mabata!sipendi hata kuwaona!kwani wanakaa wapi? Korosheni aliuliza. Yule mkulima na mkewe wakamuonyesha Korosheni pahali wanapolala mabata

wale. Korosheni aliingia ndani kujipumzisha kwani ilikuwa usiku unaanza kuingia. Korosheni aliingia chumbani kwake kulala.

Asubuhi mkulima na mke wake waliamka mapema sana. Walitayarisha chai na chakula kwa ajili ya mgeni wao. Walikaa kumsubiri Korosheni aamke. Walisubiri kwa muda mrefu lakini Korosheni hakutoka chumbani alikokuwa amelala. Yule mkulima na mke wake waliamuwa kwenda kumtazama kule chumbani. Walipofika waligonga mlango.kwa bahati mzuri mlango ulikuwa wazi.baada ya kugonga kwa muda mrefu bila majibu mkulima aliamuwa kuingia chumbani kwa korosheni.alipoingia chumbani hakumuona korosheni.korosheni alikuwa ameshaondoka.mara yule mke wa mkulima alikwenda kule kwenye banda la wale bata.hakuona bata hata mmoja.kwa hakika bata walikuwa wameibiwa.lakini nani aliiba bata?na jee korosheni yuko wapi?hayo ni maswali yaliyobaki vichwani kwa mkulima na mke wake.

KUNGURU

Hapo zamani za kale walikuwepo Kunguru. Kunguru waliishi kwa upendo na mashirikiano sana. Walifanya kazi pamoja na walisaidiana.kunguru walisshi katka nyumba na familia zao. Kila familia ilikuwa na chakula cha kutosha. Kwa miaka mingi kunguru waliishi katika maisha mazuri sana. Kunguru waliwapenda wazazi wao, wazee, na pia watoto wao.

Mwaka mmoja kulitokea ukame sana katika nchi ya Kunguru. Hakukuwa na chakula wala maji ya kutosha. Hivyo Kunguru vijana walilazimika kusafiri masafa ya mbali kutafuta chakula kwa ajili yao na wazee wao. Kunguru vizee walikuwa hawawezi kuruka kwenda mbali. Hivyo walisubiri kunguru vijana walete chakula ili wapate kula. Kunguru vijana walifanya hivyo kwa muda mrefu. Walitafuta chakula na kuchukuwa nyumbani kwa ajili ya wazee wao.

Siku moja kunguru vijana walibadili mawazo. Mmoja kati ya Kunguru hao aliwambia wenzake; ``Mnajuwa kuwa hawa wazee wameanza kuwa mzigo mzito kwetu? Kwa sababu sisi tunasafiri mbali kila siku kuwatafutia chakula. Wao hawawezi kujitafutia chochote. Hawana msaada wowote kwetu. Kwahivyo mimi naona bora tuwauwe wote ili tutafute chakula chetu tu. ` `Kunguru vijana walikubaliana kuwauwa wazee wao. Kunguru mmoja tu kijana hakuwauwa wazee wake. Yeye aliwaficha na kuendelea kuwahudumia kila siku kwa siri sana.

Njaa ilidumu kwa muda mrefu. Chakula sasa kilizidi kuwa shida kwa kunguru. Walilazimika kuruka kwenda mbali zaidi kutafuta chakula. Siku moja kunguru wakiwa wamekata tamaa ya kupata chakula walisikia kuwa chakula kinapatikana nchi za mbali.hivyo siku iliofuata waliruka kwenda huko. Safari hii iliwachukuwa siku nzima bila kufika. Walirudi nyumbani baada ya kushindwa kufika. Siku ya pili walijaribu tena

kuruka.pia walishindwa kufika kwani ilikuwa ni mbali sana. Kunguru walitumia mbinu nyingi za kuruka ilikufika nchi yenye chakula bila mafanikio.

Baada ya kushindwa kufanikiwa, mmoja kati ya Kunguru vijana alisema; ``Mnajuwa kama hatukuwauwa wazee wetu basi tusingepata shida. Wao wanajuwa mbinu nyingi ambazo zingetusaidia. Sasa mnaona tunakufa njaa bure!``. Kunguru wote waliinamisha vichwa chini na kujuta. Mmoja kati ya wale Kunguru vijana alisema;``Mimi wazee wangu sikuwauwa. Jee nikiwaleta hapa hamtowauwa? Nafikiri watatusaidia''. Kunguru vijana wote walikubali shauri lile. Yule kunguru kijana aliwaleta wazazi wake.Mzee wa kunguru alipofika aliwaambia kunguru vijana. ``Mkitaka kusafiri kwenda mbali msiruke moja kwa moja.Kwanza mnatakiwa kupaa juu zaidi mpaka muweze kuona sehemu mnayotaka kwenda.Halafu mtashuka moja kwa moja mpaka sehemu mnayotaka``.

Siku iliyofuata kunguru waliruka juu mbali sana. Baada ya muda waliweza kuiona sehemu yenye chakula chini yao. Hapo walishuka na kula chakula walichotaka.Kisha walichukuwa chakula cha ziada kwa ajili ya wazee wao waliobaki nyumbani. Kutoka siku hiyo kunguru waliweza kusafiri maeneo ya mbali na kupa chakula kwa urahisi.

MABISHANO YA VIUNGO

Siku moja viungo vilibishana baada ya kuchoka kutegeana kufanya kazi ya kuutumikia mwili. Kila kiungo kilijitapa kuwa bora kuliko chengine. Mdomo ulianza kwa kusema mimi ni bora kuliko nyinyi nyote. Kwa sababu mimi ndie ninaeweza kutamka maneno, nikasema, mkapata chakula na kuweza kunufaika.Pia kama si mimi chakula hakiwezi kupita mwilini na hivyo basi mwili mzima utashindwa kufanya kazi. Macho yakasema kumwambia mdomo; ``Wewe huwezi kuishi bila kula lakini mimi naweza. Pia nikiwa mimi sifanyi kazi mwili hauwezi kuona yanayotokea na wala kuona kitu kizuri wala kibaya. Hata chakula huwezi kukiona kama si mimi.

Kusikia hivyo masikio yakasema; ``Mimi ndio hasa ninasikiliza kila kitu na kuupa mwili ujumbe. Wakati mwengine wewe macho unaweza kuona kitu lakini wakati mwengine inawezekana huwezi kuona kitu kinachokuja hivyo ni rahisi kuuhatarisha usalama wa mwili. Kubwa zaidi mimi nakusaidia wewe mdomo kujua nini useme unapozungumza sambamba na kuufanya mwili nzima uweze kusimama vizuri bila kuyumba. Kusikia hivyo mdomo ukanyamza kimya lakini mara pua ikadaka. Pua ikaanza kwa kujisifu. Mimi ndio hasa naweza kuusaidia mwili kusikia harufu nzuri au mbaya. Kwa mfano mdomo hauwezi kuhisi kuwa chakula kinanuka aua kumechacha bila mimi kunusa chakula hicho.

Mikono nayo ikaja juu kwa kusema; mimi ndio ninatafuta kila kitu na kukipeleka kwenu. Chakula hakiendi mdomoni bila mimi kukichukuwa na kukiweka huko. Wakati mwengine masikio yanaingia wadudu au kupata uwasho. Mimi ndio nasaidia kuondoa matatizo hayo. Hata mwili unapokabiliana na maadui mimi ndio ninapanbana.Kwa upande

mwengine; mguu nao ukasema kumwambia mikono. ``Mimi ni bora kuliko wewe kwani mimi ndio nina kwenda huku na huko kuwasaidia nyinyi nyote.'' Kusikia maneno hayo kichwa kikasema mimi ndio kiongozi wenu nyote. Nikiondoka mimi tu hakuna ateweza kuishi tena. Nyote mtakufa na kusahaulika kabisa. Kusikia hivyo viungo vyote vikasalimu amri na kurejea kufanya kazi kama kawaida.

MBUZI ANAEOGOPA MAJI

Jee mnafahamu kuwa mbuzi hapendi kunywa maji? Jee mnajuwa kwanini? Babu yangu alituuliza maswali haya wakati akitusimulia hadithi na visa vya wanyama.Basi babu aliendelea. Wajukuu zangu, hapo kale alikuwepo mbuzi. Mbuzi huyo alikuwa anapenda kula majani sana.

Siku moja wakati wa kiangazi mbuzi alihisi kiu kali sana. Siku hiyo kulikuwa na jua sana. Mbuzi alitembea huku na huko kutafuta maji bila mafanikio. Kwasababu kulikuwa na jua kali wakati wa kiangazi kile, mito na maziwa mengi yalikuwa yamekauka. Mbuzi alitafuta maji huku na huko bila mafanikio.Mbuzi alikuwa amechka sana na kiu ilikuwa inazidi kuuma.Hapo aliamuwa kujipumzisha chini ya kivuli cha mti.Mara alitokea kunguru.Kunguru alimuuliza mbuzi;``rafiki yangu kwa nini unaonekana mchofu sana. Jee unaumwa?``nae mbuzi alijibu;``Hapana,mimi nina kiu sana na sijapata maji ya kunywa kabisa. ``Kunguru alimwambia mbuzi usijali nitakusaidia.

Kunguru alimwambia mbuzi amfuate ili akamuoneshe maji. Kunguru aliruka na mbuzi alifuata kivuli cha kunguru. Kunguru aliruka mbali mpaka alifanikiwa kuona ziwa moja lililokuwa na maji ya kutosha.hapo alituwa.nae mbuzi alifika hapo na kuyaona maji. Mbuzi alifurahi sana.Kunguru alimwambia mbuzi`` Rafiki yangu ingia katika ziwa unywe maji``. Mbuzi alisema;` `Asante sana rafiki yangu``. Kisha aliingia katika ziwa ili kunywa maji. Wakati anaingiza kinywa chake katika maji mbuzi alishtuka na kutoka katika lile ziwa haraka haraka. Kunguru alimuuliza mbuzi kulikoni? Mbuzi alisema. Hapana siwezi kunywa maji haya. Kwa sababu kuna mbuzi mwengine katka maji.Mimi nilipojaribu kunywa na yeye anaweka kinya chake kwenye kinywa changu. Bila shaka anataka kunidhuru!siwezi kunywa kabisa``. Mbuzi alikataa kabisa kunywa maji kwa sababu aliona kivuli chake kwenye maji. Mpaka leo mbuzi hapendi kunywa maji wala kuvuka mto wala ziwa. Pia hapendi kunywa maji kwa sababu anaogopa kivuli chake.

NGURUWE NA MVUA

Kwa nini nguruwe hapendi kujificha wakati wa mvuwa? Bibi altuuliza.Sisi sote tulikuwa hatujui kwanini nguruwe hajifichi mvua. Tulimwambia bibi ambaye alitusimulia hadithi kila siku kabla ya kulala. Bibi alianza kutusimulia. Hapo zamani za kale walikuwepo wanyama mbalimbali. Kila siku wanyama hao walikwenda kutafuta chakula sehemu mbalimbali huko msituni. Pia walitafuta maji ya kunywa.

Nguruwe alikuwa anapenda kula miwa na mihogo ya wakulima. Yeye kama kawaida yake yeye ni mnyama mkaidi, mkorofi, na mharibifu sana wa mazao ya wakulima. Kila siku nguruwe alivamia mashamba ya miwa na kula miwa mingi na kuharibu mengine. Lakini kwa muda mrefu, nguruwe alikuwa hajawahi kuona mvuwa. Kila siku alifurahia maisha ya jua na upepo mzuri katika mazingira yake.

Siku moja ilinyesha mvua nyingi na kubwa sana. Nguruwe na wanyama wengine walikimbilia sehemu zao kujificha. Sungura,na panya walikimbilia kujificha katika mashimo yao kujificha. Wanyama wengine walijificha katika majani. Nguruwe na wanyama wengine walikimbilia kujificha chini ya mti mkubwa.mti huo ulikuwa na matawi makubwa yaliyozuia mvuwa kupenya kwa wingi. Baada ya mvua kumaliza kunyesha nguruwe alibaki chini ya mti kwa muda kwani alihofia mvua nyengine kunyesha.

Wakati mvua imekwisha mti ule ulidondosha maji mengi ya mvua yaliyobaki katika majani. Hapo nguruwe alianza kurowa. Mara nguruwe alikimbia mbio na kukaa uwanjani huku akisema ``Siwezi kurowa mara mbili wakati mvuwa imenyesha mara moja. Bora nibaki hapa uwanjani bila kujificha.mara mvua nyengine ilinyesha. Nguruwe alibaki pale uwanjani na kurowa. Tangu siku hiyo nguruwe hapendi kujificha wakati wa mvuwa.

NYOTA YA JAHA

Hapo zamani za kale alikuwepo mzee mmoja aliukuwa mchoyo sana.Yeye alikuwa tajiri sana. Alikuwa na kila kitu lakini alikuwa hapendi kusaidia masikini. Pia alikuwa hapendi kumuona mtu ambae ana utajiri kuliko yeye. Siku moja alitembelea sehemu ya ng'ambo ya mji. Alipofika huko alikutana na mzee mmoja mkongwe sana. Mzee huyo alikuwa na ng'ombe mmoja tu wa maziwa. Ng'ombe huyo alimsaidia mzee huyo kupata chakula kwani alikuwa anatowa maziwa.Pia alikuwa na kuku na bata wachache. Kuona hivyo Yule tajiri alimwambia Yule mzee mkongwe amuuzie wale kuku, bata, na ng'ombe. Yule mzee alikataa na tajiri alikwenda zake.

Siku iliofuata yule tajiri alikuja tena. Alipokuja alumuona yule mzee akiwa kwenye jumba kubwa la fahari. Nje kuna walinzi,magari na mali za kila aina.Yule tajiri aliuliza; ``Jumba hili ni la nani?'' Wale walinzi walimwambia kuwa jumbe lile na la mzee mkongwe ambae alipata nyota ya jaha usiku uliopita.Yule tajiri aliona choyo sana na kusema.Hiyo nyota ya jaha inapatikana wapi?Akaambiwa baharini . Basi kabla ya kuelekezwa vizuri alikimbia na farasi wake hadi baharini. Alipofika huko akaanza kuitafuta nyota ya jaha.

Alikaa huko baharini siku nyingi akiisubiri nyota ya jaha. Baada ya siku arubaini aliamuwa kurudi bila kufanikiwa alilolitaka. Aliporudi nyumbani kwake alikuta mali zote zimeibiwa na nyumba imbomolewa yote. Akabaki hana nyumba wala mali. Tamaa na choyo vilimponza.

SHETANI

Hapo zamani za kale alikuwepo Mzee Kibwana na watoto wake wanne; Libu, Janja, Kiraka na Msafiri. Mzee kibwana alikuwa mjanja sana na mwenye vituko vya kila aina. Siku moja alikuwa anakula na watoto wake. Mara kibatari kilizimika. Mzee Kibwana aliwaambia watoto wake kuwa wasiendelee kula kizani kwani watakuwa wanakula na shetani. Watoto wa mzee kibwana wote wliogopa sana kusikia kuwa watapokula gizani watakula na shetani. Wote walisita kula mpaka hapo taa ilipowasha.

Taa ya kibatari ilipowashwa watoto na Mzee Kibwana waliendelea kula lakini waligunduwa kuwa chakula kimekuwa kikipunguwa kila taa ilpozimika. Janja; mtoto mkubwa wa mzee Kibwana alimuuliza baba yake;`` Kwanini baba hichi chakula kinapunguwa kila taa inapozimika?'' Mzee Kibwana alijibu;` `Unajuwa shetani nao ni viumbe kama sisi na hivyo basi huizima taa ili wapate kula chakula''. Baada ya kujibu swali hilo Mzee Kibwana aliendelea. Mnajuwa hawa shetani wanatuona lakini sisi hatuwaoni. Kwa hivyo hatuwezi kuwakamata kabisa.Watoto waliitikia; `Sawa.''

Siku moja , Mzee Kibwana alikuwa na watoto wake. Mara wakati wa kula ulifika. Siku hiyo kulikuwa na chakula kizuri sana. Chakula hicho kilikuwa ni pilau na nyama ya kuku. Watoto wote walikipenda chakula hicho na walitaka siku ile kibatari kisizimike kwani shetani atakula kuku wote. Baada ya kuanza kula chakula hicho watoto wote walikipenda sana. Mara taa ikazimika.Baada ya taa kuzimika Mzee Kibwana kama kawaida yake aliwaambia watoto wasiendelee kula kwani watakula na shetani. Janja

hakuamini vizuri siku ile kwani alijua kuku ataliwa tena wote. Hivyo liamuwa kupampana na shetani uso kwa uso. Janja alianza kutembeza mikono kwenye sahani. Mara alikamata mkono ukiwa ndani ya sahani. Aliukamata kwa nguvu huku akisema``Babaaa! Nimemkata shetani! Nimemkamata shetani.'' Janja alizidi kumkamata lakini alikuwa na nguvu sana yule shetani . Janja aliwaambia ndugu zake;``Nisaidieni kumshika huyu shetani ana nguvu kweli.'' Watoto wote wane walimshika vizuri shetani. Mara mama yao alikuja na taa kumuona Shetani. Alipofika na taa alishangaa kumuona mzee Kibwana kashika mkono na watoto wake wote wanne. Loh! Kumbe baba wewe ndie shetani? Watoto waliuliza kwa mshangao.

SUNGURA NA MTOTO WA MKULIMA

Hapo zamani za kale alikuwepo sungura. Sungura huyo aliishi kijijini na alikuwa na nyumba yake karibu na shamba kubwa la karanga. Sungura alikuwa hapendi kufanya kazi. Alikuwa anasubiri usiku kuiba mazao ya wakulima shambani.Kila siku sungura aliamka usiku wa manane kwenda kuiba karanga katika shamba la mkulima karibu na nyumba yake.

Mkulima alipogunduwa kuwa mazao yake yanaibiwa aliamuwa kuweka mitego katika shamba lake. Sungura hakujuwa kuwa katika shamba lile kumewekwa mitego. Usiku ulipofika tu sungura alitoka na kuingia shambani kuiba. Siku za mwizi ni arubaini. Mara

sungura alijikuta akinasa kwenye mmoja wa mitego iliokuwa humo shambani. Sungura alifanya kila mbinu ana ujanja ili atoke kwenye mtego ule bila mafaniko.

Asubuhi mkulima alifika shambani kwake na kumuona sungura akiwa amenasa katika mtego. Mkulima alifurahi sana kwa kumkamata mwizi wa mazao yake.Yule mkulima alimtoa sungura kwenye mtego na kumfunga chini ya mti. Sungura alilalamika sana ili aweze kuachwa huru. Alisema; ``Bwana mkulima mimi sio mwizi wa mazao yako.mimi nilikuwa ninapita tu humu shambani kwako. Kwa bahati mbaya nikanasa kwenye mitego hii. Tafadhali bwana mkulima niache niende nyumbani. Mimi nina mtoto mchanga na hajanyonya tangu jana. Bila shaka mtoto wangu atapata shida na hata kufariki ikiwa hutoniachia. Mkulima alimjuwa sungura vizuri. Kwa hivyo alimwambia``wewe sungura ni mjanja sana.Lakini leo huna njia ya kujitetea.Kitabu chako cha ujanja kimefika tamati leo. Lazima nile nyama yako!``

Kusikia vile Sungura alishindwa na la kusema. Alikaa pale chini ya mti akisubiri hukumu. Saa sita mchana mtoto wa mkulima alikuja pale shambani. Yule mkulima alimwambia yule mtoto wake;``Mchukuwe huyo sungura umpeleke nyumbani. Mwambie mamako amchinje na kumpika. Tutakula nyama ya sungura leo. Sawa?``mtoto aliitikia ``sawa baba.'' Yule mtoto alimchukuwa sungura na kwenda nae nyumbani. Mtoto alitembea kwa miguu. Kwa vile nyumbani kwa yule mkulima ni mbali mtoto alitembea muda mrefu kabla ya kufika nyumbani. Katlkati ya safari sungura alimuuliza yule mtoto;

``Jee bado unakumbuka ulivyoagizwa na baba yako?'' Yule mtoto alisema; ``Ndio ninakumbuka.Baba kaniagiza nimwambie mama akuchinje ili tule nyama ya sungura.'' Kusikia vile, sungura alicheka sana! Ha! Ha! Haaaa! Umesahau ulivyoagizwa. Baba yako atakugomba sana kwa kusahau maagizo yake. Sungura alimwambia yule mtoto.

Mtoto alimuuliza sungura. Jee unakumbuka baba alivyoniagiza? Sungura alisema ndiyo. Basi niambiae. Sungura akamwambia; ``Hapana! Mimi sikwambii kwa sababu ulikuwa humsikilizi baba yako. Yule mtoto kusikia vile alikaa chini ya mti na kumuomba sungura amwambie.

Baada ya muda mrefu kupita, sungura alimwambia yule mtoto ambaye kwa sasa alikuwa analia. Sungura alimwambia yule mtoto. ``Tafadhali usilie. Mimi nitakukumbusha alivyokuagiza baba yako.'' Mtoto alifurahi na kumsikiliza sungura. Sungura alianza kwa kusema''. Baba yako amesema umwambie mama yako kuwa amchinje huyo jogoo mkubwa kwa ajili ya chakula changu mimi mgeni. Umefahamu? Sungura alihoji. Mtoto nae alisema ndio nimefahamu. Hivyo alimchukuwa sungura na walipofika nyumbani mtoto alimpa mama yake maagizo aliyopewa na sungura. Mama wa yule mtoto alimtayarishia chakula kizuri yule sungura. Sungura alikula chakula na kwenda zake. Mkulima aliporudi aliona nyama ya kuku badala ya sungura.